



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb: Na. HWC/L.20/03/VOL/VIII/62/ARR

21.03.2024

**MKURUGENZI MTENDAJI,
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC),
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.**

**YAH: UTHIBITISHO WA UMILIKI WA MASHAMBA KIJIKI CHA KWEIKONJE
CHALINZE KWA MWEKEZAJI RODEENA LIMITED**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu pamoja na barua yako yenye Kumb.Na.CA.148/234/01G/36 ya tarehe 29/02/2024.

Tunapenda kukutaarifu kuwa tarehe **17.11.2023** ofisi ilipokea barua kutoka kwa Mtendaji wa kijiji cha Kweikonje akiitambulisha kampuni tajwa hapo juu ambayo imeonesha nia ya kuwekeza katika kijiji chao ambapo kijiji kilipokea maombi ya kumilikishwa eneo lenye ukubwa wa ekari 497.

Mtendaji wa Kijiji alieleza kuwa Kampuni ya **RODEENA LIMITED** ya **S.L.P 21487, DAR ES SALAAM**, hapa nikiirejea kama kampuni ya kigeni ambayo inawakilishwa na ndugu **MADONGO ABDALLA HEMEDI** (Mtanzania aliyepewa nguvu za kisheria) inaomba kumilikisha shamba lenye ukubwa wa **ekari mia nne tisini na saba (497)** kwa ajili ya kilimo cha **Ufuta**

Kampuni ya **RODEENA LIMITED** ilipata eneo hilo kutoka kwa Wananchi wazawa wapatao **ishirini na nne (24)** katika kijiji cha Kweikonje. Kampuni hiyo ililipa stahili za Wananchi hao kwa kuzingatia makubaliano yaliyowekwa kati ya wananchi na kampuni tajwa na baadaye kuwasilisha ombi la umilikishaji kwenye Halmashauri ya kijiji hicho.

Baada ya kampuni kukamilisha taratibu za kupipa stahili za wamiliki asili, maombi ya kumiliki ardhi hiyo yalijadiliwa na Halmashauri ya kijiji tarehe **09.11.2023** na mapendekezo ya kikao cha Halmashauri ya kijiji yaliwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Kweikonje uliofanyika tarehe **10.11.2023** ambapo kwa mujibu wa **Sheria ya Ardhi ya kijiji sura ya 114**, kijiji kilipendekeza mwombaji apewe eneo hilo lenye ukubwa wa **ekari 497** ambapo mwekezaji atapaswa kufanya yafuatayo kwenye kijiji:

- (a) Kuingiza umeme kwenye Zahanati ya kijiji jambo ambalo ameshalitekeleza
- (b) Kujenga nyumba ya daktari na hili alisema atalitekeleza desemba 2025
- (c) Kumalizia ujenzi wa ofisi ya kijiji na alihaidi atalitekeleza desemba 2024
- (d) Kumalizia ujenzi wa jengo la ibada (msikiti, jambo ambalo ameshatekeleza ombi hilo
- (e) Kujimba kisima kirefu kwenye senta ya kijiji na jambo hili alihaidi atalitekeleza katika mwaka wa fedha **2025/2026**
- (f) Kukarabati bwawa la maji la kwa Mhando na alisema atalitekeleza Julai 2024 na
- (g) Kwa wakulima waliopo jirani na shamba la mwekezaji; alihaidi kuwalimia kwa mkopo na kuwapatia mbegu bora ya zao la ufuta na watamuuzia Rodeena Limited kwa kuzingatia bei ya soko la ufuta

Kwa kuwa ukomo wa ugawaji ardhi ngazi Halmashauri ya kijiji ni ekari 50; Halmashauri ya Wilaya ilipokea muhtasari wa kijiji ukipendekeza kummilikisha mwekezaji Rodeema Limited kwa mujibu wa sheria.

Baada ya kupokea maombi hayo, timu ya wataalam ilifanya ukaguzi tarehe 25/01/2024 na tulibaini yafuatayo:

- (a) Uweo wa eneo lenye ukubwa wa ekari 497 ambapo eneo lenye ukubwa wa ekari 430 limesafishwa kwa ajili ya kilimo kusudiwa
- (b) Uwepo wa wafanyakazi na wataalam wa kilimo
- (c) Uwepo wa vitendea kazi kama Wheel loader, bulldozer na tractor na

Kwa sababu hizo, tunapenda kudhibitisha kuwa eneo hilo ni mali ta Kampuni ya Rodeena Limited ambaye amenunua kutoka kwa Wananchi wazawa wapatao ishirini na nne eneo lenye jumla ya ekari 497.


Pili tunadhhibitisha kuwa tarehe 25.01.2024 ofisi ilikaga eneo hilo na haikubaini mgoro wowote wakati wa ukaguzi.

Pamoja na barua hii, nimeambatisha mikataba ya manunuzi, mihtasari ya vikao vyote viwili vilivyojadili na kuridhia maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa Sheria

Naomba kuwasilisha kwa hatua zinazofuata.



Ramadhani Possi
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
CHALINZE**



Nakala kwa: RODEENA LIMITED

S.L.P 21487,

DAR ES SALAAM (kwa taarifa na ufuatiliaji).

Mtendaji wa Kijiji Cha Kweikonje (kwa taarifa)